

ASb  
approved



# Akai Amefurahi

Translators without Borders

Rob Owen

Kiswahili





Akai hakuwa na viatu. Marafiki zake walivaa viatu vizuri walipocheza.




Akai alimwomba mamake amnunulie viatu. Ilikuwa shida kucheza bila viatu.



Walipotembea kijijini, mama alitambua kuwa watoto wengine walivaa viatu isipokuwa Akai na Etabo.



Siku moja asubuhi mama alimwamsha Akai. Alimwambia  
ajitayarishe waende sokoni.



Akai na mamake walitembea hadi sokoni.



Walipoingia katika duka la viatu, Akai alifurahi sana.



Usiku ule, Akai hakuweza kulala. Aliwazia tu viatu vyake vipya.






Hamu ya kuvaa viatu ilizidi. Akai akasimama na kuvivaa viatu vyake.



Hata baada ya kurudi kitandani, Akai aliwaza jinsi angewaonyesha wenzake viatu vyake.



Akai aliamka tena na kuvivaa viatu vyake vipya akacheza cheza chumbani.



Mama aliingia chumbani. Alimpata Akai amelala kitandani akiwa amevaa viatu. Akamwambia Akai asivivae tena viatu vyake kitandani.



Akai alifurahi kupata viatu kwa mara ya kwanza.

You are free to download, copy, translate or adapt this story  
and use the illustrations as long as you attribute in the  
following way: Ursula Nafula Author - Ursula Nafula  
Translation - Translators without Borders and Pete Mhunzi  
Illustration - Rob Owen  
Language - Kiswahili  
Level - First sentences © African Storybook Initiative 2015  
Creative Commons: Attribution 4.0  
Source [www.africanstorybook.org](http://www.africanstorybook.org)

